More past papers are available on http://www.kenyaplex.com

Form 4 Mock 102/3 KISWAHILI Past Paper

102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI 3
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA 2 ½

TATHMINI LA PAMOJA WILAYA YA BUTERE – 2010
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E.)

102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI 3
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA 2 ½

MAAGIZO

?Jibu maswali manne pekee.
?Swali la kwanza ni la lazima.
?maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Ushairi, Hadithi Fupi na Tamthilia.
?Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa.
FASIHI SIMULIZI
1. LAZIMA
a) Eleza maana ya maigizo katika fasihi simulizi. (alama 2)
b) Taja sifa tano za maigizo katika fasihi simulizi.(alama 10)
c) Eleza umuhimu wa maigizo katika fasihi simulizi.(alama 8)

USHAIRI
Jibu swali la 2 au 3

2. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake ni moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakizifuata nyago
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurahi shaitani, bali tajawa chukizo
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo
Tamko lake 'subutu', kuondoa tumaini, na kukuuliza wazo
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui

Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Kwa hakika ni balaa, kumkivimu mchawi, aliye jaa uchoyo
Bahati ina hadaa, kukupa alo sodawi, aibatili rohoyo
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaniyo
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Ninacho changu kilio, nalia sanasana, kinyesi nimetupiwa
Ningetoa azimia, lakini uwezo sina, kwa mazito kuambiwa
Ama nitimue mbio, fuadini ninanena, akilini na zuiwa
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

MASWALI

a) Eleza dhamira ya shairi hili.(alama 2)
b) Eleza muundo wa shairi hili.(alama 4)
c) Huku ukitoa mifano, eleza aina mbili za idhini ya kishairi alizotumia mshairi.(alama 4)
d) Andika ubeti wa mwisho katika lugha ya nathari.(alama 4)
e) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo:
i) Ni kiumbe chenye zani.(alama 1)
ii) Kukupa alo sodawi.(alama 1)
f) Taja na ufafanue mbinu mbili za lugha alizotumia mshairi.(alama 4)
3. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:
Ndugu zangu nauliza / naomba kuelezwa
Neno hili lina kisa, lanishinda kuelewa
Nawasaili wajuza, wenye kujua kuzuwa
Nini mana mtumwa,, wenzangu wenye kujua?

Wenzangu wenye kujua, haja yangu mshajuwa
Nipeni mwezi na jua, nipate kupambanuwa
Kwani nimeyachagua, nipotwa kuyafichuwa
Nini mana ya mtumwa, wenzangu wenye kujua?

Pengine huwa nadhali, mtumwa ni mti kuwa
Tena hilo naamini, nakiri nalitambuwa
Sote tulo viumbwani, tu watumwa wenye kujua?
Nini ma’na ya mtumwa, wenzangu wenye kujua?

Fakhari yangu jamani, ni utumwa kutumiwa

Kwa Rabuka mhisani, muumba mwenye kujuwa
Pili ni huko kazini, Taifa taka jengewa
Nini mana ya mtumwa, wenzanguu wenye kujua ?

Tatu ni wangu wazazi, kwao mtumwa mekuwa
Si jambo lenye kuhizi, bali la kufurahiwa
Kutumwa si pingamizi, huenda mbio kwa hatuwa
Ninin ma'na ya mtumwa, wenzangu wenye kujua?

Nne huja ya dunia, ya kutamani madawa
Kila jambo kupimia, na watu kuchaguliwa
Vyeo kuvipigania, kazi hudharauliwa
Nini ma'na ya mtumwa, wenzangu wenye kujua ?

Mapenzi yakitishika , mengi husauliwa
Hata kama ni kuzika , rahisi kuachiliwa
Mradi twafurahika, akili kupunguziwa
Nini ma'na ya mtumwa, wenzangu wenye kujua?

Pia ninaukataa, wa unafiki fanyiwa
Ya kushikwa kama kaa, na mtu ati ajuwa
Walau si yetu taa, asiwe aabudiwa
Nini ma'na ya mtumwa, wenzangu wenye kujua?

Mwafrika kujitoa, lazima nyongo kutowa
Asiwe ajipodoa, kwa picha kufotolewa
Ya utumwa kuhomoa , na upumbavu kutiwa
Nini ma'na ya mtumwa, wenzangu wenye kujua?

Mwanagenzi nasimama, naomba kuachiliwa
Ingawa hayajakoma, yangu niloyafichuwa
Nimefika hatima, jawabu zangojelewa
Nini ma'na ya mtumwa wenzangu wenye kujua?

Maswali
a)Fafanua falsafa ya mshairi kuhusu utumwa .( alama 4)
b)Andika ubeti wa nane kwa lugha ya nathari.(alama 4)
c)Taja na ufafanue bahari nne kuu ambazo shairi hili laweza kuanishwa.(alama 4)
d)Eleza maana ua msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi.

(i)thawabu ( alama 1)
(ii)Mumbuwa ( alama 1)
e)Taja mifano miwili ya matumizi ya tabdila na inkasari.(alama 2)

RIWAYA

S.A MOHAMMED : Utengano

Jibu swali la 4 au 5

4.“Voti zenu zinastahiki mtu mwenye sifa nilizotaja. Mnahitaji mtumishi kama mimi....

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b)Fafanua sababu za mzungumzaji kusema wanahitaji mtumishi kama yeye.(alama 6)

c)Taja na ueleze tamathali mbili za lugha zinazodhihirika katika dondoo hili.(alama 4)

d)Ni kwa ninin jumuiya ya utengano haihitaji mtumishi kama mrejelewa .(alama 6)

5.Huku ukitumia mifano kumi eleza jinsi mwandishi wa utengano alivyotumia majazi (alama 20)

HADITHI FUPI

K.W WAMITILA : mayai waziri wa maradhi.

6.Huku ukirejelea hadithi zozote tano husika katika diwani ya mayai waziri wa maradhi eleza wazo kuwa utekelezaji wa mfumo wa elimu umekumbwa na changamoto nyingi.(alama 20)

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA : Kifo kisimani.

7.“ Mara nyingi vijana hushughulika mambo ya kibinafsi. Mara nyingi mawazo yao hufuata mkondo wa anasa za vijana .....

a)Eleza muktadha wa usemi huu.(alama 4)

b)Mwandishi ameshughulikiaje mchango wa vijana katika uchanya na uhasi
Fafanua .(alama12)

c)Eleza hatima ya mazungumzo haya.(alama 4)